# LEARNING BY EAR 2011

## "The Promised Land - A Story of African Migration to Europe"

## EPISODE FIFTEEN: "Reverse Migration"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: CHIVASI ARRIVES AT THE TRAIN STATION IN THE CAPITAL**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Information desk worker (m, 50)**
- **Linda (f, 20)**

**SCENE TWO:**

- **Farahani (m, 19)**

**SCENE THREE: CHIVASI AT LINDA'S PARENTS IN THE EVENING**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Linda (f, 20)**

- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingene ya Noa Bongo Jenga Maisha yako.Hii ni sehemu ya 15 na ya mwisho kwenye mfululizo wa mchezo huu **“Ardhi ya Ahadi- hadithi kuhusu Waafrica wanahamia Ulaya.”.** Katika kipindi kilichotangulia, Linda anampigia simu Mamake usiku wa manane kumuomba msamaha, lakini hakumuleza zaidi kosa alilofanya.Na baada ya kutoroka kuzuizini, Chivasi, amekuwa akifanya kibarua katika bustani ya maua ya Bwana Ralph bila ya kibali. Na wakati Ralph anapokataa kumlipa, anatorokea nyumbani kwa Rhoda. Rhoda anakubali kumpa nauli ya kumpelekahadi jijini Linda anakosomea. Na huko Kizuizini,hatimaye Farahani,amefanikiwa kupata hifadhi kama mkimbizi wa Ulaya, lakini haamini anachoambiwa kuhusu sheria za mkimbizi huko Ulaya.Miongoni mwa sheria hizo ni kwamba hawezi kufanya kibarua chochote cha kulipwa mshahara. Hii ndio pazia ya hadithi yetu!.Na je nini utakaokuwa mwisho wa rafiki zetu na ndoto zao za kuhamia Ulaya? Endelea kuwa nasi katika sehemu hii ya mwisho**“Kubadili nia ya uhamiaji”.** Na tunaanza na Chivasi akiwa katika kituo cha gari moshi karibu na chuo kikuu ambako anakwenda katika meza ya huduma ya kuwaelekeza wageni ili apate maelekezo zaidi.

**<u>SCENE ONE: CHIVASI ARRIVES AT THE TRAIN STATION IN THE CAPITAL</u>**

1. **SFX: EUROPEAN TRAIN STATION ATMO**

2. **CHIVASI:** Habari. Unaweza kunielekeza kufika Chuo kikuu? Nataka kwenda kufika kitivo cha uanasheria wa kiimataifa.?

3. **INFO. MAN:** Samahani, hapa ni kituo cha gari moshi na sio ofisi ya watalii, na kazi yetu ni kuwaelekeza abiria kuhusu ni wakati gani Garimoshi litawasili au kuondoka,na nauli inayopasa kulipwa. Ukitaka kuelekezwa au rahamani ya jiji naomba ufike katika ofisi ya maelezo kwa watalii.

4. **CHIVASI:** **(adamant - at the end of his tether)** Sikiliza!, Nimeteseka muda mrefu. Kwa hiyo tafadhali nisaidie kunielekeza kama unafahamu!. Kwanini hutaki kunisaidia! Kwani nafanana na kuwa mtalii? Sikuja hapa kutalii! Usiniambie niende kwa ofisi ya habari ya idara ya Utalii.

5. **INFO. MAN:** **(nervous)** Sawa,sawa… Si mbali kutoka hapa kwenda chuo kikuu!. Ukitoka nje ya kituo, pinda kushoto, uende hadi mwisho wa barabara, kisha pinda kulia na kufuata barabara kuu, baada ya mwendo wa dakika tano hivi, utakiona Chuo kikuu.

6. **CHIVASI:** Ahsante sana kwa usaidizi wako. Kwaheri na uwe na siku njema. **(aside)** Wazungu na sheria zao za kusumbua…

7. **NARRATOR:** Chivasi anahema baada ya kukimbia katika barabara inayoelekea chuo kikuu,na sasa yuko hatua chache tu kukutana na mchumba wake Linda Maraga. Walinzi wa mlangoni wanamwelekeza chumba anamoishi Linda. Kumbukumbu za tangu utotoni zinamjia anapopanda ngazi kuelekea chumbani mwake. Na muda si muda anafika chumba nambari 316, na mlangoni anakutana jina la: Linda Maraga.

8. **SFX: GENTLE KNOCKING ON DOOR**

9. **LINDA:** Ni nani?

10. **SFX: SAME GENTLE KNOCKING ON DOOR**

11. **LINDA:** Sawa, sawa.

12. **SFX: DOOR BEING UNLOCKED**

13. **CHIVASI:** **(softly)** Hujambo mpnezi wangu!

14. **LINDA:** **(total shock and disbelief)** Chivasi! Ni wewe! Siamini! Umefika - ! Wewe..-

15. **CHIVASI:** **(still soft)** Nimevuka bahari kwa ajili yako tu mpenzi Linda! Kumbuka nilivyokuahidi. Nipite

ndani?

**16. LINDA:** **(in tears)** Oh mungu,! Oh Mungu … Umefika! Yaani umefika Ulaya. Umefika vipi huku? Chivasi… Pita ndani, karibu ndani! Niko na mengi sana ya kukueleza.

**17. CHIVASI:** Kweli? Pia mimi nina hadithi ndefu sana ya kukueleza…

**18. NARRATOR:** Chivasi na Linda wanaanza kuhadithiana kuhusu masaibu waliyopitia wakiwa Ulaya. Chivasi anasikitishwa na kisa kilichompata Babake Linda, huku naye Linda anasikitishwa sana na mambo yaliyomkuta Chivasi katika juhudi zake kutaka kuungana naye Ulaya. Hatimaye anaamua kumwambia ukweli hukusu ndoa yake bandia na Charles ili aweza kupata kibali cha kufanya kazi Ulaya. Lakini anashukuru Mungu kwani sasa hayo yamepita. Asubuhi hiyo alikuwa amepata barua kumfahamisha kwamba ndoa yao na Charles imefutiliwa mbali.

**19. LINDA:** **(regretfully)** Pole sana, Chivasi. Samahani sana kwa kukufanya upitie mambo haya yote, na muda huo wote nilikuwa nimefunga ndoa na Mtu mwengine, sikuwahi hata kukuelezea. Sistahili penzi lako tena! Nilidhani nilichokuwa nikifanya kitanisaidia maishani! Hata hivyo sijakuwa na uhusiano wowote wa kimapnzi na Charles ingawa nilisaliti penzi lako tu! Samahani sana. Lakini sasa

tuko pamoja tunaweza kuanza maisha upya.... Hii ni barua imetoka mahakamani na inafutilia mbali ndoa hiyo.

**20. CHIVASI:** **(bitter)** Lakini kwanini, Linda? Uuuuh, Kwanini? Unliahidi kwamba tutaoana. Kwanini ukaamua kufunga ndoa na mtu mwengine?

**21. LINDA:** **(breaking down)** Ilinibidi kufanya hivyo! Sikuwa na jinsi! Nilihitaji pesa kujikimu…Ohhhh..,Chivasi, samahani … tafadhali nisamehe!.

**22. CHIVASI:** Sasa nitajiwasilisha kwa maafisa wa uhamiaji Linda. Sijui kama watanifanya nini? Lakini sitaki wanipeleke gerezani. Bora wajirejeshe nyumbani Afrika. Nilikutana na mtu mwengine ambaye alinishauri niwe makini sana na kila jambo ninalofanya. Nadhani sasa wakati huo umewadia.

**23. LINDA:** Chivasi – Unataka tuoane?

**24. CHIVASI:** Linda – Usiniulize swali hilo sasa! Nimechanganyikiwa sana! Sijui nataka nini tena maishani mwangu? Lakini najua nataka kurudi nyumbani. Ukitaka tunaweza kuandamana.

**25. NARRATOR:** Nini maoni yako? Je Chivasi aendelee na mipango ya kumuoa Linda hata baada ya yote yaliyotokea? Siku chache baadaye, Chivasi anajiwasilisha kwa maafisa wa uhamiaji, akiwa na hakika

kwamba atarudishwa nyumbani Africa. Wakati huo huo Farahani anahamishwa hadi kambi ya wakimbizi, ambako ndoto ya maishani mwake inaaza kutimia. –Maisha ya ukimbizi.…

**SCENE TWO: FARAHANI AT THE REFUGEE CENTRE**

**26. SFX: SAD MUSIC**

**27. FARAHANI:** Haya siyo mambo niliyodhania kabisa.Hapa sina uhuru!. Nilidhani nitaanza kufanya kazi punde tu nitakapowasili Ulaya. Lakini yaonekana ndio mwanzo mkoko unaalika maua! Niko na marafiki wengi sana hapa!. Sistahili kuishi maisha haya! Na siwezi kurudi nyumbani. Nitachekwa.! Ni sawa tu niishi hapa. Labda wakati nitakapopewa chumba changu mambo yatabadilika. Sijui lakini ni lini mambo haya yatatokea. Mbali na hayo hapa nilipo sina pesa- na itanichukua muda kabla nianze kufanya kazi.

**28. NARRATOR:** Farahani ameghadhabishwa sana na ukweli wa mambo kuhusu ndoto yake ya kuhamia Ulaya.Tukirudi Africa, Chivasi amerudi nyumbani na kuendelea na shughuli zake za kawaida. Lakini maisha si rahisi kwani Linda bado yuko Ulaya, na watu wanamuona mjinga kurejea nyumbani baada ya kufika Ulaya.! Kejeli zinazidi kuongezeka katika mitandao ya kijamii na analazimika kufunga ukurasa wake wa Facebook. Sasa anaelekea nyumbani kwa wazazi wa Linda kumjulia hali Babake Linda ambaye anaendelea kupata nafuu baada ya kuhusika kwenye ajali ya barabarani na pia kumuelezea jinsi watu

wanavyomsimanga.

**SCENE THREE: CHIVASI AT LINDA'S PARENTS IN THE EVENING**

**29. SFX: EVENING ATMO IN AN AFRICAN NEIGHBOURHOOD**

**(Light laughter from Chivasi, Mr & Mrs Maraga)**

**30. CHIVASI:** Ni kweli, watu wanafikiri mimi ni wazimu kwa sababu niliamua kurudi nyumbani Afrika.

**31. MRS. MARAGA:** Siwezi kukulaumu.

**(More laughter from them)**

**32. MR. MARAGA:** **(coughs)** Kitu ambacho sijaelewa, kwanini kupitia mateso yote hayo na hatimaye kukutana na Linda huko Ulaya, kisha hapa unasema huko tayari kumuoa? Au nakosea?

**33. CHIVASI:** **(mumbles, embarrassed)**

**34. MRS. MARAGA:** Chivasi, nafurahi sana kwamba unaendelea vizuri. Ni vyema uchukue likizo kazini upumzike, kwani ingekuwa vigumu kutafuta kazi nyingine kama ungeipoteza kazi yao.

**35. CHIVASI:** Ni kweli. Lakini naamini kwamba bado kuna nafasi nyingi sana hapa Barani Africa ambazo hazijatumika kikamilifu. Nashangaa kwanini watu

hung’ang’ania kwenda kwingineko ambako tayari kunaustawi? Kwanza tustawisha hapa nyumbani Afrika!

**36. MR. MARAGA:** Pia sisi tumekuwa na mawazo sawa na yako, lakini tukafahamu kwamba yalikuwa mawazo tasa!. Ni kweli Africa kuna nafasi nyingi na nzuri sana za kujistawisha, lakini nafasi hizi zinatolewa kwa wachache wetu tu. Hebu fikiria kama si Linda kwenda Ulaya nani angeweza kugharamia matibabu yangu hospitalini.?

**37. CHIVASI:** Samahani sana Bwa Maraga, lakini hilo sikubaliani nawe kamwe. Nadhani ingekuwa bora zaidi kama Linda angekamilisha masomo yake ya chuo kikuu hapa nyumbani. Hapa pia angeweza kuajiriwa kazi nzuri katika kampuni inayotoa huduma za kisheria. Au pengine hata angekuwa ameanza kujisimamia yeye mwenyewe na kuanzisha kampuni yake ya uanasheria.

**38. MRS. MARAGA:** Kampuni ya kisheria za kimataifa? Na wateja angewapata kutoka wapi?

**39. CHIVASI:** Oh, hilo halingekuwa tatizo. Hebu tazama hizi kesi za wanasiasa hapa Africa, na mfano viongozi wanaofikishwa katika mahakama ya kimataifa huko ‘The Hague’. Mahakama hiyo bado imefungua ofisi nyingi sana hapa Afrika. Amini usiamini hawa mawakili hulipwa pesa nyingi sana.

**40. MR. MARAGA:** Hapo umesema ukweli, Chivasi. Lakini bado nafurahi kwamba ameenda ng'ambo. Ingawa masomo yake yametugharimu sana.

**41. SFX: DOG BARKING LOUDLY OUTSIDE**

**42. MRS. MARAGA:** Kwani tunatarajia mgeni mwengine?

**43. MR. MARAGA:** Mimi sina habari. Ni usiku sana kupokea wageni. Chivasi hebu chungulia ni nani anayebisha mlangoni?

**44. CHIVASI:** Bila shaka.

**45. SFX: METAL DOOR BEING UNLOCKED**

**46. LINDA:** Hujambo, mpenzi wangu…

**47. CHIVASI:** **(surprised)** Linda! Unafanya nini hapa?

**48. MRS. MARAGA:** Linda! Ni wewe?

**49. MR. MARAGA:** Eti?! Linda amerudi?

**50. LINDA:** Humjambo.Ndiyo nimerudi!.Kama mtaridhia!.

**51. CHIVASI:** Yaani unataka kusema umerudi nyumbani – hutarudi tena Ulaya? Na je masomo yako?

**52. LINDA:** Nataka kumaliza masomo yangu hapa nyumbani nikiwa karibu na watu ninao wapenda na wanaonipenda pia. Baba unaendeleaje?

**53. MR. MARAGA:** Nini? Naendelea vizuri…! Unamaana unataka kukamilisha masomo yako hapa nyumbani? Imesalia mwaka na nusu kukamilisha masomo yako!

**54. LINDA:** Baba samahani sana kama nimekukosea. Lakini nimeamua kwamba nitakamilisha masomo yangu hapa nyumbani.

**55. MRS. MARAGA:** **(furious)** Kwani haya ndiyo Chivasi alikwambia alipokuwa huko Ulaya? Kuacha maisha yako ya Ulaya na kurudi katika bara hili lililojaa maovu? Kufanya nini? Ili nyinyi wawili muweze kuoana na wewe kuishia Mama Jikoni?

**56. CHIVASI:** Nini?!!

**57. LINDA:** Mama tafadhali usisema hivyo.Kamwe haya haya muhusu Chivasi! Sivyo unavyofikiria! Kwa taarifa yako, ningefurahi sana kama unayosema yangekuwa ya kweli.

**58. MR. MARAGA:** Tosha, punguzeni hasira,. Ndio mwanzo Linda amewasili nyumbani, baada ya safari ndefu. Lazima

amechoka na anahitaji kupumzika. Tunaweza kuyazungumza haya kesho asubuhi. Karibu nyumbani binti yangu. Tunafurahi umefika salama.

**59. CHIVASI:** Sasa naomba kuondoka. Bila shaka mnahitaji muda wa kuzungumza na Linda. Linda karibu sana nyumbani!.

**60. LINDA:** Asante sana Chivasi, Tafadhali funga mlango na unisubiri kidogo kuna mambo ningetaka kumfahamisha Baba na Mama, ambayo pia wewe yanakuhusu!. Wakati umewadia pia mimi kutenda yale yanayostahiki.

**61. SFX: METAL DOOR BEING LOCKED**

**OUTRO:**

Chivasi anafunga mlango wa mbele na kumsikiliza Linda… Na hadi hapo tunafika mwisho wa sehemu hii ya 15 na ya mwisho kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio**“Ardhi ya Ahadi- hadithi kuhusu Waafrica wanaohamia Ulaya.”.** Je unadhani nini kitakatokea kwa Linda, Chivasi na Farahani? Unadhani Florence na Charles wanafaa kuachiliwa huru au kufungwa gerezani? Lakini la muhimu zaidi, nini maoni yako kuhusu uhamiaji kuelekea Ulaya na masuala yote yaliyojitokeza kwenye mchezo huu.? Na pia ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw-.de/destinationeurope.Na ni hayo tu kutoka kwetu hadi tutakapokutana tena kwaheri